

JIMBO KATOLIKI LA SUMBAWANGA
PAROKIA YA FAMILIA TAKATIFU-TUNDUMA
SHULE YA SEKONDARI MT. KAROLO BOROMEO
TAARIFA YA SHULE YA SEKONDARI MT.KAROLO
BOROMEO

- JINA LA SHULE: SHULE YA SEKONDARI MT. KAROLO BOROMEO
- NAMBA YA USAJILI:S 5089
- KATEGORI YA SHULE: NI SHULE YA BWENI KWA JINSI ZOTE YAANI WASICHANA NA WAVULANA
- MAWASILIANO KWA UTAWALA WA SHULE
 - MKUU WA SHULE: 0766659974
 - MAKAMU MKUU WA SHULE: 0768108715/0622923959
 - MHASIBU: 0754359363
 - BARUA PEPE: mtkaroloboromeo@gmail.com
- MAZINGIRA YA SHULE KWA UJUMLA:

- **JENGO LA UTAWALA**



- **MAKTABA YA SHULE**



- **MADARASA YA KIDATO CHA KWANZA MPAKA CHA NNE**



- **JENGO LA MAABARA**



- **BWALO LA CHAKULA**



- **MABWENI YA WANAFUNZI WA KIKE NA KIUME**



➤ **HISTORIA FUPI YA SHULE:**

- ✓ Shule ya sekondari Mt. Karolo Boromeo ni shule inayomilikiwa na Jimbo katoliki la Sumbawanga chini ya Baba Paroko wa Parokia ya Familia Takatifu –Tunduma. Shule imesajiliwa vema kwa vigezo na matakwa ya Baraza La Mitihani La Tanzania na kupewa namba ya Usajili kama kituo cha mitihani kwa namba **S5691**. Wazo na chimbuko la kujenga shule hii lilianzishwa na Baba Paroko Padri VITUS VICTORY KASUNGA mwanzoni mwa mwaka 2013 ambapo wazo hili lilifahamishwa kwa viongozi na waamini wa Parokia ya Familia Takatifu-Tunduma na mara moja zoezi la maandalizi ya ujenzi yakaanza katika eneo la kanisa ambalo linapatikana katika kigango cha chipaka. Jiwe la msingi la kuanza ujenzi liliwekwa na Mhashamu Baba Askofu, DAMIAN KYARUZI mnamo 30/07/2014. Masomo yalianza rasmi tarehe 07/01/2019 na mnamo tarehe 27/07/2019 Makamu wa Mhasham Baba Askofu, Baba MODESTUS KATONTO aliizindua rasmi kwa niaba ya Mhasham Baba Askofu Baba BEATUS URASSA ambapo shule ilianza na wanafunzi 96 wa kidato cha kwanza na mpaka sasa mwaka 2023 shule ina idadi ya wanafunzi 348 .

➤ **MWENENDO WA KITAALUMA WA SHULE**

- Kimsingi shule tangu kuanzishwa kwake kwa Neema ya Mwenyezi Mungu imekuwa ikifanya vizuri sana kwenye eneo la kitaaluma katika mitihani ya

ndani na nje ya shule kwa ngazi za kiwilaya, kimkoa, kikanda na kitaifa kwa ujumla.

- Tukiangazia matokeo ya shule kwa ngazi ya kitaifa tangu imeanza kufanya mitihani ya kitaifa kwa kidato cha pili na kidato cha nne yamekuwa kama ifuatavyo.

❖ **MATOKEO YA KIDATO CHA PILI MWAKA**

-MWAKA 2020

IDADI YA WANAFUNZI ILIKUWA=86

- ✓ DARAJA LA KWANZA=85
- ✓ DARAJA LA PILI=01
- ✓ DARAJA LA TATU=00
- ✓ DARAJA LA NNE=00

-MWAKA 2021

IDADI YA WANAFUNZI ILIKUWA= 84

- DARAJA LA KWANZA =80
- DARAJA LA PILI=04
- DARAJA LA TATU=00-
- DARAJA LA NNE=00

-MWAKA 2022

IDADI YA WANAFUNZI ILIKUWA =65

- DARAJA LA KWANZA=51
- DARAJA LA PILI=14
- DARAJA LA TATU=00
- DARAJA LA NNE=00

❖ **MATOKEO YA KIDATO CHA NNE MWAKA 2022**

IDADI YA WANAFUNZI ILIKUWA =80

- ✓ DARAJA KWANZA =27
- DARAJA LA PILI=48
- DARAJA LA TATU=05
- DARAJA LA NNE=00

❖ **TAMATI:**

- Katika kufanikisha haya yote katika mlengo wa kitaaluma mkazo umekuwa hasa kwenye kujikita zaidi katika sala kwa kila shughuli yoyote inayofanywa kwa waalimu na wanafunzi ndani na nje ya madarasa pamoja na kujikita zaidi kwenye kuimarisha nidhamu ya wanafunzi pamoja na wafanyakazi.

➤

TUMSIFU YESU KRISTU

